ISSN 2820-2686 | Toleo Na. 5 | Julai - Desemba 2022

# JARIDA LA WAKILI MKUU







osgtanzania osg_tanzania WAKILI MKUU TV Email: info@osg.go.tz www.osg.go.tz

# BODI YA UHARIRI


## Mwenyekiti

Sarah Duncan Mwaipopo

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

Prisca Jackson Ulomi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

Sarah Obby Mwakyusa

Afisa Habari Mwandamizi

Dennis Julius Buyekwa

Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

Nyamhoni Robert Chacha

Afisa TEHAMA

## Wajumbe

George Nathaniel Mandepo

Mkurugenzi wa Usuluhishi

Hangi Matekeleza Chang'a

Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

Kiuye Mbwana Shemakame

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

CPA Devota Mathew Ngulugulu

Mhasibu Mkuu

Mercy Rowland Kyamba

Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

Zuhura Mohamed Kussaga

Mchumi

# Tahariri ya Mhariri



## Prisca Jackson Ulomi

### Mhariri Mkuu

## Hongera Dkt. Luhende na Bi. Mwaipopo kwa Kuteuliwa Kuongoza OWMS

Tarehe 10 Oktoba, 2022; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwateua Dkt. Boniphace Nalija Luhende kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali.

Natumia fursa hii, kuwapongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia kushika nafasi hizo za uongozi na tunaamini ya kwamba mtakwenda kusimamia umoja na mshikamano katika Ofisi hii ili kuhakikisha malengo ya Ofisi yanafikiwa kwa mujibu wa Mpango Mkakati.

Akihutubia mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika mwezi septemba mwaka jana mkoani Dodoma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwafananisha Mawakili wa Serikali kama wahandisi kwa kucheza na vifungu vya sheria.

Mhe. Dkt. Samia aliwasihi Mawakili wa Serikali kujiweka vizuri katika kusimamia na kulinda uwekezaji unaofanyika nchini Tanzania kwa sababu unakwenda kupanua wigo na kukuza uchumi.

Ni ukweli usiopingika kuwa katika zama za sasa Mawakili wa Serikali wakitumika kimkakati watatusaidia kulinda uchumi, uwekezaji na biashara kwa kutumia kalamu za sheria ili nchi iendelee kupokea wawekezaji na maslahi yapatikane kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.

Tunafurahi kuona kuwa Mawakili wa Serikali wanaendelea kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na uadilifu wakizingatia uzalendo na kuweka mbele maslahi mapana ya taifa kwa ujumla pasipo kukiuka haki za wananchi, kuendelea kulinda uwekezaji nchini na kupanua wigo wa kukuza uwekezaji.

Tunawasihi Mawakili wa Serikali kuendelea kuharakisha kusikiliza migogoro ya uwekezaji kwa njia ya majadiliano ili kuepuka migogoro inayotokea mara kwa mara kwa lengo la kupunguza idadi ya wawekezaji na wafanyabiashara kwenda mahakamani kufungua mashauri.

Aidha, tunapongeza jitihada kubwa zinazofanywa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kuona haja na umuhimu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na ushirikiano wa karibu na Ofisi hiyo katika utekelezaji wa majukumu kwa kuwa na vikao vya pamoja vya mara kwa mara vya ngazi ya viongozi na watendaji wengine ili kuhakikisha kuwa majukumu ya Ofisi tajwa yanatekelezwa kwa wakati, ufanisi na kuongeza tija.

Ofisi hizi mbili ni kiungo muhimu katika kuisadia Serikali kufikia malengo yake ikiwemo ya kuwaletea wananchi maendeleo, pia ni Ofisi ambazo mambo mengi na mazito yanapita na ni mambo ambayo wakati mwingine yanahitaji ushauri wa haraka au maamuzi ya haraka hivyo ushirikiano na mawasiliano kati ya Ofisi hizi ni jambo ambalo halikwepeki.

Ni matumaini yetu kuwa Mawakili wa Serikali wataendelea kuishauri vema Serikali na taasisi zake kuhusu namna bora ya kumaliza migogoro na wananchi au wawekezaji bila kuathiri maslahi ya nchi.

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Sarah D. Mwaipopo**

**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

## Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Toleo la Tano la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali ni maalumu kwa ajili ya kuangazia uelekeo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inapoelekea kutimiza miaka mitano tangu kuanzishwa kwake. Katika kuangazia hilo, jarida hili linaendelea kutambua mchango mkubwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha Ofisi hii. Pamoja na mchango mkubwa wa Mhe. Rais, Ofisi ya Wakili Mkuu imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuhakikisha tunaendelea kuiwakilisha vyema na kwa weledi mkubwa katika uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi hii, toleo hili litajumuisha matukio yote muhimu yaliyofanyika katika kipindi cha miezi sita ikihusisha mabadiliko ya kiuongozi katika Ofisi hii na uteuzi wa viongozi mbalimbali katika Ofisi uliofanywa na Mhe. Rais Dkt. Samia. Pia, toleo hili litaangazia suala la ushirikiano wa Ofisi mama za Sheria yaani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika utendaji kazi wake ikiwa ni pamoja kujenga vituo jumuishi katika mikoa mbalimbali nchini. Toleo hili limegusia ushiriki wa Mawakili wa Serikali kwenye vyombo vya kitaaluma vya Mawakili ikiwemo Chama cha Mawakili wa Serikali (Public Bar Association-PBA) kilichozinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Septemba, 2022.

Pamoja na mafanikio mengi, toleo hili litatoa muendelezo wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambapo tayari ujenzi umeanza na unaendelea kupitia mkandarasi SUMA JKT na mshauri elekezi Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Mambo haya na mengine mengi yataakisiwa ndani ya jarida hili.

Naomba nimalizie kwa kuomba wasomaji waendelee kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri kwa ajili ya maboresho na maoni kuhusu jarida hili. Kwa pamoja tutaweza kulifanya jarida kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Sekta ya Sheria hapa nchini.

Nawatakia usomaji mwema wa toleo la tano la Jarida la Wakili Mkuu.

Asanteni

# Yaliyomo


06 RAIS SAMIA AZINDUA CHAMA CHA MAWAKILI WA SERIKALI

10 UTEUZI WA VIONGOZI WA OFISI

16 MAWAKILI ZINGATIENI MASLAHI MAPANA YA NCHI

19 SERIKALI YAENDESHA MASHAURI 6,043 YA MADAI NA USULUHISHI

22 TUMEPEWA DHAMANA YA KUITETEA SERIKALI

24 WAZIRI NDUMBARO AWEKA JIWE LA MSINGI JENGO JUMUISHI

29 DKT. LUHENDE: MAJUKUMU YAZINGATIE TARATIBU

32 WATENDAJI TUMIENI MAWAKILI WA SERIKALI

34 BARAZA KUWEKA MAHALA PA KAZI SEHEMU SALAMA

36 TUWAJIBIKE KWA PAMOJA KWA MASLAHI YA TAIFA

39 OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI, TIArb KUSHIRIKIANA

43 SERIKALI KUENDELEZA SEKTA YA SHERIA NCHINI

46 OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KIGOMA YAPATA GARI



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akibonyeza Kitufe kuashiria uzinduzi wa mfumo rasmi wa Kieletroniki wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OAG-MIS), nembo ya Ofisi hiyo pamoja na Chama cha Mawakili wa Serikali katika Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali uliofanyika Septemba, 2022 Jijini Dodoma.*

# Rais Samia Azindua Chama cha Mawakili wa Serikali

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa Mawakili wote wa Serikali ambao hawajasajiliwa kwenye rejista ya Mfumo wa Taarifa wa Mawakili wa Serikali kujisajili kabla ya muda kupita ili watambulike kwenye Mfumo wa Kieletroniki wa Taarifa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujulikanao kwa jina la OAG-MIS.

Mhe Rais Dkt. Samia aliyasema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali kabla ya kuzindua Chama cha Mawakili wa Serikali (Public Bar Association) uliofanyika kwenye Ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma wenye kauli mbiu isemayo, "Utekelezaji wa Majukumu Unaozingatia Sheria ni Nyenzo Muhimu kwa Maendeleo ya Taifa".

"Amri inapotoka Wanasheria wajisajili na muda umetolewa kama mtu hajajisajili awe na dharura ya maana sana, aidha alikuwa mgonjwa hospitalini hawezi au alikokuwa hakuna mtandao hakupata taarifa kwa wakati, kama muda utapita na usajili hajafanya basi Mwanasheria Mkuu nakutaka kusimamia hilo", alisema Mhe. Rais.

Mhe. Rais alimtaka Mwanasheria Mkuu wa

Serikali kuwahimiza wale ambao bado hawajajisajili, wajisajili kwenye mfumo wa OAG-MIS vinginevyo baada ya muda kupita hawatatambulika kama Mawakili wa Serikali na itabidi watafute sekta za nje wajisajili au kupewa msamaha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Rais Dkt. Samia alipongeza uanzishwaji wa Chama cha Mawakili wa Serikali cha kitaaluma na kusema uwepo wake utasaidia zoezi la kuratibu utendaji kazi wa Mawakili wote wa Serikali walio katika utumishi wa umma nchini na amewaeleza kuwa wamepata mlezi mzuri ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali anayeweza kuwasemea katika masuala yao ya kitaaluma, kikazi, kinidhamu na kimaslahi.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Viongozi mbalimbali pamoja na Mawakili wa Serikali kabla ya kuzindua Chama cha Mawakili wa Serikali, nembo na Mfumo rasmi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika hafla iliyofanyika Septemba, 2022 Jijini Dodoma.*

"Lakini nimefurahishwa kusikia kwamba Chama hiki kilichoundwa kitafanya kazi kwa karibu na Chama cha Mawakili cha Tanganyika (TLS) pia nimefurahishwa na kusikia uhusiano wa karibu wa kazi baina yenu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar", alisema Mhe. Rais Dkt. Samia

Aidha, alisema itakuwa ni rahisi kuwasiliana kupitia mfumo huo wa Mawakili wa Serikali ambao ameuzindua na kusema ni dhahiri maboresho hayo yataongeza ari na tija kwa Mawakili wa Serikali wanapotekeleza majukumu yao katika maeneo mbali mbali nchini.

Akimkaribisha Mhe. Rais, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro alisema mkutano huo ulitanguliwa na kikao kazi cha Wakuu wa Idara na Vitengo vya Sheria wa Wizara, Taasisi, Idara na Halmashauri zote nchi nzima na kuelezwa kuhusu mpango wa kuanzisha Chama cha Mawakili wa Serikali.

Dkt. Ndumbaro alisema chama hiki kitakuwa



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akitembelea mabanda mbalimbali likiwemo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kujionea shughuli mbalimbali pamoja na huduma zitolewazo na Ofisi hizo kabla ya kuhutubia na kuzindua Rasmi Chama cha Mawakili wa Serikali, nembo na Mfumo rasmi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*

kikisimamia masuala ya kitaaluma na masuala ya kimaadili ya Wanasheria na ni fursa nzuri ya kutoa changamoto za kimaadili ambazo zimekuwa zikiwakabili na itawezekana tu kama Mhe. Rais Dkt. Samia atakubali ombi la kuzindua chama hicho.

"Mhe Dkt. Samia, kupitia Chama cha Mawakili wa Serikali tunatarajia kwamba chama hiki kitaleta umoja wenye nguvu na jukwaa mahsusi kabisa la kuishauri Serikali katika mambo mbalimbali ya kisheria na tunatarajia kwamba litakuwa ni sehemu ya majadiliano ya kisheria kwa wanasheria wa Serikali ambalo lilikosekana huko nyuma". alisema Dkt. Ndumbaro.

Aliwakumbusha Mawakili wa Serikali kwamba, kuwa Wakili wa Serikali ni heshima kubwa na heshima ya kuwa Wakili inaendana na wajibu hivyo wanapaswa kuitumikia Serikali ipasavyo na kutumia sheria kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza ndani ya Serikali.

Awali Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi aliwataka watendaji wa Serikali kuhakikisha wanawatumia vizuri Mawakili wa Serikali waliopo kwenye rejista ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupata ushauri kabla hawajaingia kwenye mikataba au kabla ya kuvunja mikataba ili wazingatie kanuni na taratibu.

Jaji Dkt. Feleshi alisema chama kitakuwa ni jukwaa la Mawakili kujadili masuala mbalimbali ya kisheria yakiwemo ya kimafunzo yanayohusiana na utoaji wa huduma za kisheria na kutatua malalamiko ya kisheria kutoka kwa wadau mbalimbali.

Naye Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bw. Msalama Mkama aliishukuru Serikali kwa kuwa na maono ya mbali na kuanzisha Chama cha Mawakili wa Serikali ambacho kitakuwa kama jukwaa kwa Mawakili hao kujadili masuala yao ya msingi kwenye Sekta ya Sheria.

Bw. Mkama alisema kuwa chama hicho kitaiwezesha Serikali kuwaunganisha Mawakili na kujadili changamoto zao kwa pamoja na kuiwezesha Serikali kufahamu idadi na utendaji kazi wa Mawakili katika Wizara, Taasisi, Sekretariati za Mikoa na Halmashauri zote nchini.

"Chama kitawawezesha Mawakili kushirikishana katika ujuzi walio nao na kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi katika kusimamia mashauri ya Serikali kutoka kwenye taasisi zao na pia kutatua changamoto walizonazo kwa kutumia uzoefu walio nao". alisema Mkama.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende, Mkurugenzi wa Mashtaka, Slyvester Mwakitalu, viongozi waandamizi wastaafu wa Sekta ya Sheria nchini akiwemo Mtemi Andrew Chenge.



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisalimiana na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende mara baada ya kuwasili kwenye ukumbi wa mikutano wa Jakaya Mrisho Kikwete, Dodoma kwa ajili ya kuzindua Chama cha Mawakili wa Serikali Septemba, 2022.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiwa kwenye banda la maonesho la Ofisi hiyo wakati wa uzinduzi wa Chama cha Mawakili wa Serikali jijini Dodoma Septemba, 2022.*



*Baadhi ya Wakurugenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (walioketi mbele) wakimsikiliza kwa makini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi Mkutano na uzinduzi wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika jijini Dodoma Septemba, 2022.*

# Uteuzi wa Viongozi wa Ofisi



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Dar es Salaam*
*10 Oktoba, 2022*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Wakili Mkuu wa Serikali na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kama ifuatavyo:

1) Amemteua Dkt. Boniphace Christopher Luhende kuwa Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu Dkt. Luhende alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Dkt. Luhende anachukua nafasi ya Bwana Gabriel Paschal Malata ambaye aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

2) Amemteua Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu Bi. Mwaipopo alikuwa Wakili wa Serikali Mkuu katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Bi. Mwaipopo anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Dkt. Luhende ambaye ametuliwa kuwa Wakili Mkuu wa Serikali.

Uteuzi huu umeanza tarehe 09 Oktoba, 2022.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

# Rais Samia Ateua Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewateua viongozi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali hatua itakayosaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Dkt. Samia amemteua Dkt. Boniphace Nalija Luhende kuwa Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu Dkt. Luhende alikuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Dkt. Luhende anachukua nafasi ya Bw. Gabriel Pascal Malata ambaye aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

Aidha, Dkt. Samia amemteua Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya Uteuzi huu Bi. Mwaipopo alikuwa Wakili wa Serikali Mkuu katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Bi. Sarah Duncan Mwaipopo anachukua nafasi ya Dkt. Boniphace Nalija Luhende ambaye ameteuliwa kuwa Wakili Mkuu wa Serikali.

Uteuzi huu umeanza tarehe 09 Oktoba, 2022.



**Dkt. Boniphace N. Luhende**
**Wakili Mkuu wa Serikali**



**Sarah D. Mwaipopo**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Dkt. Boniphace Nalija Luhende kuwa Wakili Mkuu wa Serikali katika hafla iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 22 Oktoba, 2022. (Picha na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu)*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali katika hafla iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 22 Oktoba, 2022. (Picha na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu)*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Mbeya*

*06 Agosti, 2022*

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameteua maafisa ishirini na wawili (22) kuwa Majaji wa Mahakama Kuu tarehe 04 Agosti, 2022 kama ifuatavyo:-

1. Kevin David Mhina, kabla ya uteuzi huu Bwana Mhina alikuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani;
2. Gabriel Pascal Malata, kabla ya uteuzi huu Bwana Gabriel alikuwa Wakili Mkuu wa Serikali;
3. Adrian Philbert Kilimi, kabla ya uteuzi huu Bwana Adrian alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
4. Happiness Philemon Ndesamburo, kabla ya uteuzi huu Bi. Happiness alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
5. Victoria Mlonganile Nongwa, kabla ya uteuzi huu Bi. Victoria alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
6. Obadia Festo Bwegoge, kabla ya uteuzi huu Bwana Obadia alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
7. Ruth Betwel Massam, kabla ya uteuzi huu Bi. Ruth alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
8. Godfrey Ntemi Isaya, kabla ya uteuzi huu Bwana Godfrey alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
9. Gladys Nancy Barthy kabla ya uteuzi huu Bi. Gladys alikuwa Naibu Msajili wa Mahakama;
10. Haji Suleiman Haji, kabla ya uteuzi huu Bwana Haji alikuwa Mwendesha Mashitaka Mfawidhi Mahakama Kuu, Zanzibar;

11. Fatma Rashid Khalfan, kabla ya uteuzi huu Bi. Fatma alikuwa Kamishna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
12. Abubakar A. Mrisha, kabla ya uteuzi huu Bwana Abubakar alikuwa Wakili wa Serikali;
13. Lusungu Hemed Hongoli, kabla ya uteuzi huu Lusungu alikuwa Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
14. Monica Peter Otaru, kabla ya uteuzi huu Bi. Monica alikuwa Mkurugenzi Msaidizi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
15. Kamana Stanley Kamana, kabla ya uteuzi huu Bwana Kamana alikuwa Mkurugenzi Msaidizi (TAMISEMI);
16. Hamidu Rajabu Mwanga, kabla ya uteuzi huu Bwana Hamidu alikuwa Mkurugenzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
17. Marlin Leonce Komba, kabla ya uteuzi huu Bi. Marlin alikuwa Mkurugenzi wa Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;
18. Dkt. Mwajuma Kadilu Juma, kabla ya uteuzi huu Dkt. Mwajuma alikuwa Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu Mzumbe;
19. Dkt. Cleophas K.K. Morris, kabla ya uteuzi huu Dkt. Cleophace alikuwa Mhadhiri, Chuo Kikuu Dar es Salaam;
20. Asina A. Omari, kabla ya uteuzi huu Bi. Asina alikuwa Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC);
21. Aisha Zumo Bade, kabla ya uteuzi huu Bi. Aisha alikuwa Wakili wa Kujitegemea; na
22. Mussa Kassim Pomo, kabla ya uteuzi huu Bwana Mussa alikuwa Wakili wa Kujitegemea.

Tarehe ya uapisho wa Majaji Wateule itatangazwa baadaye.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

*Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhe. Gabriel Pascal Malata kuwa Jaji wa Mahakama Kuu katika hafla fupi iliyofanyika viwanja vya Ikulu, Chamwino Jijini Dodoma Agosti, 2022. (Picha na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu)*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhe. Abubakar Amini Mrisha kuwa Jaji wa Mahakama Kuu katika hafla fupi iliyofanyika viwanja vya Ikulu, Chamwino Jijini Dodoma Oktoba, 2022. (Picha na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu)*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Hangi Matekeleza Chang'a kuwa Kamishna wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika hafla liyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma Oktoba, 2022. (Picha na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu)*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (Mb) akizungumza na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa kikao chake cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kilichofanyika Agosti, 2022 jijini Dar es Salaam.*

# Mawakili Zingatieni Maslahi Mapana ya Nchi

Serikali imeitaka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kuzingatia maslahi mapana ya nchi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku ya kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ili kuhakikisha kuwa inatetea maslahi ya Serikali na wananchi ndani na nje ya nchi

Hayo yalielezwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) wakati wa kikao kazi baina yake na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliyoongozwa

na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Nalija Luhende kilichofanyika mwezi Agosti, 2022 kwa lengo la kuwa na majadiliano na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ili kujadili utekelezaji wa majukumu.

Dkt. Ndumbaro alisema kuwa ni muhimu Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ihakikishe inaiwakilisha vema Serikali na taasisi zake kwenye mashauri ya madai na usuluhishi ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata inachostahili kwa maslahi mapana ya taifa na wananchi kwa ujumla ili kulinda hadhi ya Serikali.

"Wizara hii imeshikilia haki ya wananchi; amani na utulivu wa nchi; na uwekezaji nchini; hivyo ni muhimu kuhakikisha wananchi wanapata haki zao kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi zilizopo; nchi inavutia wawekezaji kwa kuhakikisha amani na utulivu; pamoja na kuwa na miongozo stahiki inayohusu mikataba katika uwekezaji ili kulinda maslahi mapana ya taifa," alifafanua Dkt. Ndumbaro.

Aliongeza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa maslahi mapana ya taifa la Tanzania hivyo ni muhimu kwa watumishi kutekeleza majukumu kwa kuweka uzalendo mbele; kuzingatia taaluma; maadili ya kazi; weledi na uzoefu kwenye maeneo ya migogoro, usuluhishi na majadiliano ikiwa ni pamoja na kushirikisha wadau ili kuhakikisha kuwa Serikali inashinda na kunufaika na uwepo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji ya Ofisi kwa niaba ya Menejimenti, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Luhende alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa Ofisi hiyo mwaka 2018 hadi mwezi Juni mwaka 2022; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha jumla ya mashauri 5,905 ambapo kati ya hayo mashauri 5,768 ni ya madai na mashauri 137 ni ya usuluhishi.

Dkt. Luhende aliongeza kuwa ili kufikia azma ya kupanua wigo wa utendaji wa Ofisi hiyo na kuongeza ukaribu katika kuhudumia wananchi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina Ofisi 17 ambazo zimefunguliwa kwenye mikoa yote yenye masjala za Mahakama Kuu ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kwenye mikoa ya Dodoma; Mtwara; Iringa; Ruvuma; Tanga; Kilimanjaro; Arusha; Kigoma; Mara; Mwanza; Kagera; Shinyanga; Tabora; Rukwa; Mbeya; na Morogoro.

Dkt. Ndumbaro akiwa Dar es Salaam kwenye ziara ya kikazi alionana na kuzungumza na taasisi za Wizara ikiwemo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Tume ya Haki za Binadamu; Wakala wa Vizazi na Vifo; na Taasisi ya Msaada wa Kisheria ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo kwa Serikali kwa niaba ya wananchi



*Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza kwa makini Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (hayupo pichani) wakati wa kikao cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kilichofanyika jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damasi Ndumbaro (Mb) (aliyesimama mbele katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kikao kazi na Ofisi hiyo kilichofanyika mwezi Agosti, 2022 jijini Dar es Salaam.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Dkt Damasi Ndumbaro akiteta jambo na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt Luhende (kushoto) baada ya kumaliza kikao chake na Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika mwezi Agosti, 2022 jijini Dar es Salaam.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na wajumbe wa Baraza la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) wakati akifungua Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 uliofanyika mwezi Septemba, 2022 jijini Dodoma.*

# Serikali Yaendesha Mashauri 6,043 ya Madai na Usuluhishi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) imeendelea kuiwakilisha Serikali katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi ambapo imefanikiwa kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi 6,043 kwa kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018.

Hayo yalielezwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende wakati akizindua kikao cha kwanza cha Baraza la pili la wafanyakazi wa OWMS lililofanyika mwezi

Oktoba, 2022 jijini Dodoma na kusema kuwa OWMS imeendesha mashauri hayo kwa niaba ya Serikali kwa umakini mkubwa na umahiri ili kuendelea kutekeleza majukumu ya OWMS ili kufikia na hata kuzidi matarajio ya Serikali.

Aliongeza kuwa OWMS imeendelea kuiwakilisha Serikali Mahakamani na katika mabaraza ya usuluhishi ambapo tangu kuanzishwa kwake imeendesha mashauri ya madai yapatayo 5,885 na mashauri ya usuluhishi 158 na kufanya jumla ya mashauri kuwa 6,043.

"Mashauri ya madai yaliyomalizika katika kipindi cha miaka minne ni mashauri 582 na ya usuluhishi ni mashauri 60 ambapo kati ya hayo, Serikali imeshinda mashauri 530 ya madai na Mashauri ya usuluhishi 31", alisema Dkt. Luhende

Alisema kuwa kama alivyoagiza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, OWMS imeendelea kuhakikisha inaiwakilisha vyema Serikali na kuvutia wawekezaji nchini kwa kumaliza migogoro mbalimbali dhidi ya wawekezaji na wafanyabiashara kwa njia ya majadiliano jambo ambalo limesaidia kupunguza idadi ya migogoro dhidi ya Serikali iliyofunguliwa kwenye Mahakama na mabaraza nje na ndani ya nchi; kuokoa fedha za Serikali ambazo zingetumika katika kuendesha migogoro tajwa; kudumisha uhusiano kati ya Serikali na wawekezaji; kujenga imani kwa wawekezaji kuhusu hali ya utoaji haki nchini; na kukuza diplomasia ya uchumi.

"Mfano wa shauri la usuluhishi lililomalizika kwa njia ya majadiliano ni baina ya G.S Engineering & Construction Corporation ya Korea ya Kusini dhidi ya TANROADS likihusiana na ujenzi wa daraja la Tanzanite mgogoro ulikuwa umepelekwa ICC na shauri lilimalizika na sasa daraja linaendelea kutoa huduma kwa wananchi," alisema Dkt. Luhende.

Pia, aliwapongeza watumishi wa OWMS ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa ufanisi ili kuhakikisha maslahi ya Taifa yanalindwa pamoja na kukuza diplomasia ya uchumi wa nchi.

Mmoja wa wajumbe wa Baraza hilo, Wakili wa Serikali, Bw. Rashid Mohamed alisema siri ya mafanikio yaliyopatikana ni uongozi thabiti wenye kutoa maelekezo sahihi ya namna ya kutekeleza majukumu ya Ofisi ambapo Mawakili wenyewe wamekuwa na jitihada za kujifunza kile wanachokifanyia kazi ili kuweza kuleta mafanikio kwenye kazi wanazozifanya.

Naye Wakili wa Serikali Mwandamizi, Bi Jenipher Kaaya ambaye pia ni mjumbe wa Baraza hilo alisema kuwa OWMS inafanikiwa kumaliza mashauri nje ya mahakama au mabaraza ya usuluhishi kwa kufanya majadiliano na wale wanaoidai Serikali kwa kuweka masuala ya kisheria pembeni na kujadili hoja kama watu wa kawaida na hatimaye kufika muafaka na



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiimba wimbo maalumu wa Mshikamano Daima wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi hiyo uliofanyika Septemba, 2022 jijini Dodoma.*

kuweza kushinda mashauri hayo.

“Katika majadiliano hayo kuna sehemu kadhaa tunatumia sheria kwa kutegemeana na aina ya kesi na hivyo kwa kutumia usuluhishi tumefanikiwa kumaliza migogoro mingi kwa wakati na kwa muda mfupi tofauti na mahakamani ambapo historia inaonyesha kuwa migogoro inakaa mwaka mmoja au miaka miwili mpaka kumalizika,” alifafanua Bi. Kaaya.

Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa OWMS, James Kibamba alitoa rai kwa wajumbe hao kuhakikisha kuwa wanawakilisha vema watumishi wengine na kuwapatia mrejesho kwa kuwa sio rahisi kwa watumishi wote kuwa wajumbe wa Baraza.



*Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Zuhura Kussaga (kulia) akiwa na aliyekuwa Naibu Katibu wa Baraza hilo, Adam Muchuzi (kushoto) wakati wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo uliofanyika Septemba, 2022 jijini Dodoma.*



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ufunguzi wa Baraza hilo uliofanyika Septemba, 2022 jijini Dodoma.*

# Tumepewa Dhamana ya Kuitetea Serikali



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (kulia) akimkabidhi Bi. Sarah Mwaipopo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali nyaraka za uendeshaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara walipowasili kwenye Ofisi hiyo kufanya makabidhiano na kuzungumza na watumishi kwenye Ofisi hiyo Oktoba, 2022 jijini Dar es Salaam baada ya kuteuliwa kwao na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa hizo.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imepewa dhamana ya kuitetea Serikali na taasisi zake kwenye mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi ili kulinda maslahi mapana ya Taifa kwa ujumla.

Kauli hiyo ilitolewa na Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende wakati akizungumza na Menejimenti na wafanyakazi wa OWMS mara baada ya kuapishwa kutumikia cheo hicho.

Dkt. Luhende aliwataka watumishi hao kuendelea kupambana na kusimamia haki, sheria na kulinda mali za Serikali kama alivyosema Mhe Rais kuwa Mawakili ni mainjinia wa haki.

"Katika kipindi hiki ambacho Mhe. Rais wetu anafanya jitihada kubwa sana katika kuvutia wawekezaji nchini, sisi kama Ofisi inayosimamia mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa dhidi au kwa niaba ya Serikali tuna jukumu la kuhakikisha kuwa haki inatendeka ili kudumisha imani kwa wawekezaji," alisemea Dkt. Luhende.

Alieleza kuwa kusimamia haki kutasaidia kumaliza migogoro kwa wakati na kwa kufuata haki na sheria, kudumisha uhusiano kati ya Serikali na wawekezaji, kujenga imani kwa wawekezaji kuhusu hali ya utoaji haki ili kukuza diplomasia ya uchumi nchini.

Dkt. Luhende aliwataka watumishi kutekeleza majukumu yao kwa bidii, uwazi, uwajibikaji, uadilifu na ueledi kwa maslahi mapana ya Taifa na kuendelea kudumisha umoja na ushirikiano ili kuhakikisha wanaitetea Serikali kwa ufanisi na kuwa mstari wa mbele katika kujenga uchumi wa nchi.

Akimkaribisha Wakili Mkuu wa Serikali, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Duncan Mwaipopo aliwataka Wakuu wa Idara na Vitengo kutekeleza majukumu ya Ofisi na

kutambua kuwa wote wana wajibu wa kusimamia vema rasilimali watu na fedha kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma ili kuwa na utendaji wenye tija, kuleta matokeo makubwa na ufanisi kwa lengo la kuendelea kujenga taswira nzuri iliyopo kwa wadau, wananchi na taifa kwa ujumla.

"Ni imani yangu kuwa kila mmoja wetu atasimama katika nafasi yake na kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia taaluma aliyonayo, ujuzi, uzoefu na kulinda maslahi mapana ya taifa letu huku tukizingatia dhana ya uwazi, uwajibikaji, na kufanya kazi kama familia moja kwa kuwa tunatumia muda mwingi kuwa Ofisini tukitekeleza majukumu yetu hivyo ni muhimu kuendelea kudumisha umoja, upendo na mshikamano," alisema Bi. Mwaipopo.



*Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) alipowasili kwenye Ofisi hiyo na kukabidhi nyaraka za uendeshaji wa Ofisi hiyo Oktoba, 2022 jijini Dar es Salaam.*

# Karibu



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akikabidhiwa ua na Bw. Athumani Zunda, Mtumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipowasili kwa mara ya kwanza kwenye Ofisi hiyo baada ya kuteuliwa na kuapishwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo.*



*Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (aliyeketi kushoto), Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, James Kibamba wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi hiyo Oktoba, 2022 jijini Dar es Salaam baada ya viongozi hao kuwasili Ofisini hapo baada ya kuteuliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nyadhifa hizo.*

# Waziri Ndumbaro Msingi Jengo




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro baada ya kuweka jiwe la msingi la jengo jumuishi la taasisi za sheria lililopo eneo la Buswelu wilayani Ilemela mkoani Mwanza Novemba, 2022. Kutoka kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt. Khatibu Kazungu, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi.*

# Aweka Jiwe la Jumuishi



Ujenzi kugharimu shilingi bilioni 3.8, kukamilika ndani ya miezi 18

Yasogeza huduma za kisheria na utoaji haki karibu na wananchi

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) ameweka jiwe la msingi kwenye jengo jumuishi la taasisi za kisheria linalojengwa eneo la Buswelu Wilayani Ilemela mkoani Mwanza ambapo jengo hilo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudumia watumishi 70 wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Waziri Dkt. Ndumbaro alisema kuwa ujenzi wa jengo hilo utasogeza huduma za kisheria na utoaji wa haki karibu na wananchi hivyo mwananchi atapata huduma za kisheria sehemu moja na huduma za ustawi wa jamii na msaada wa kisheria.

Vile vile, aliongeza kuwa ujenzi huo utagharimu shilingi bilioni 3.8 na unatumia fedha za ndani ambazo ni kodi za wananchi na huu ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ambayo inaitaka tasnia ya sheria nchini kuwapa wananchi haki ya kisheria kwa karibu, haraka na gharama nafuu.

Alisema kuwa Serikali itaendelea kujenga majengo jumuishi nchi nzima kwa kila mkoa ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu mbalimbali na kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuhudumia wananchi kwa kuwa taasisi za kisheria ni taasisi za utoaji haki hivyo ni muhimu kuimarisha miundombinu husika.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Khatibu Kazungu alisema kuwa majengo jumuishi yameonesha faida kwa watumishi kwa kufanya kazi kwa pamoja na yanajenga mahusiano mazuri baina ya taasisi za kisheria.

Naye Mwanasheria Mkuu



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akimkaribisha Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (wa kwanza kushoto) alipowasili kuweka jiwe la msingi jengo jumuishi la taasisi za sheria lililopo eneo la Buswelu wilayani Ilemela mkoani Mwanza Novemba, 2022. Wa pili kushoto anayefurahi ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi.*

wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi alisema kuwa matumizi ya pamoja ya fedha yamefanyika kwa kutumia fedha za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambapo fedha za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka zimetumika kununua kiwanja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inagharamia ujenzi wa jengo hilo.

Mhe. Jaji Dkt. Feleshi alisema kuwa uwepo wa jengo jumuishi utawezesha huduma zinazotolewa kupatikana katika eneo moja kwa kuwa Ofisi hizi zinategemeana katika utoaji huduma za kisheria kwa wananchi na itapunguza gharama kwa wateja kwa kuwa watakuwa wanapata huduma mahali pamoja.

Akizungumza kwa niaba ya Mshauri Elekezi wa ujenzi wa jengo hilo kutoka Wakala wa Majengo Tanzania, Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri, Msanifu Majengo Wencelaus Kizaba alisema kuwa hadi sasa mkandarasi wa jengo hilo, SUMA JKT tayari alilipwa shilingi 885,422,794.72 kati ya shilingi bilioni 3.8 na TBA ambaye ndiye mshauri elekezi alilipwa shilingi 32,468,435 na ujenzi umefikia kiwango cha asilimia 35% na ni wa muda wa miezi 18 ambapo hadi sasa imetumika miezi



*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (wa kwanza kushoto) akipata maelezo ya michoro ya ujenzi wa jengo jumuishi la taasisi za sheria kutoka kwa Msanifu Majengo wa TBA, Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri, Wencelaus Kizaba wakiwa eneo la ujenzi wa jengo hilo Buswelu wilayani Ilemela mkoani Mwanza Novemba, 2022.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sarah Mwaipopo (aliyeketi wa kwanza kulia) akimsikiliza Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (hayupo pichani) wakati akihutubia kabla ya kuweka jiwe la msingi la jengo jumuishi la taasisi za sheria linalojengwa eneo la Buswelu lililopo wilayani Ilemela mkoani Mwanza Novemba, 2022.*

saba na mkataba uliingiwa tarehe 19 Aprili, 2022 na ujenzi unatakiwa kukamilika tarehe 25 Oktoba, 2023.

Alifafanua kuwa ujenzi umetoa ajira kwa watanzania, wanafunzi wamepata mafunzo kwa vitendo na ununuzi wa vifaa vya ujenzi unafanyika kwa kununua bidhaa kutoka soko la ndani hivyo Serikali inapata mapato.

Akitoa salamu kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, ndugu Hassan Masala alisema kuwa uongozi wa Mwanza uko tayari kuendelea kusimamia ujenzi huo ili kuona ufanisi wa miradi mikubwa ya Serikali na watashirikiana na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ili Serikali iweze kufikia malengo iliyojiwekea.

Uwekaji huo wa jiwe la msingi ulihudhuriwa na viongozi mbali mbali akiwemo Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende, Mkurugenzi wa Mashtaka, Silyvester Mwakitalu, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sarah Mwaipopo, Mkabidhi Wasii Mkuu wa RITA, Angela Anatory, Naibu Msajili Mkuu wa Mahakama Kuu – Mwanza, Chiganga Tebwa, Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; viongozi wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Ilemela, viongozi wa Tarafa, Kata, Mtaa na wananchi kwa ujumla.




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (wa tatu kushoto) na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (wa pili kushoto) wakijiandaa kukagua ujenzi wa jengo jumuishi la taasisi za sheria wakiwa eneo la ujenzi Buswelu wilayani Ilemela mkoani Mwanza Novemba, 2022.*



*Picha ya muonekano wa jengo jumuishi la taasisi za sheria linalojengwa eneo la Buswelu wilayani Ilemela mkoani Mwanza kwa ajili ya matumizi ya watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wa mkoa huo.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Mawakili wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki kikao kilichofanyika kwa njia ya mtandao kwenye ukumbi wa Ofisi hiyo kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Ofisi kilichofanyika Desemba, 2022 jijini Dar es Salaam.*

# Dkt. Luhende: Majukumu Yazingatie Taratibu

Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) wamekumbushwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kufuata utaratibu unaofaa hatua itakayosaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ili kufikia malengo waliyojiwekea kwa wakati.

Wito huo ulitolewa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende wakati akifanya kikao kwa njia ya mtandao na Mawakili wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali waliopo Dar es Salaam na wale wa mikoani kwa lengo la kujadili na kukumbushana mambo mbalimbali yanayohusu OWMS kwa lengo la kuboresha na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Dkt. Luhende alisema kuwa kufuata utaratibu kutasaidia sana kuboresha huduma zinazotolewa na Ofisi hiyo hasa katika suala la uendeshaji wa mashauri ya Serikali

ambayo ndio jukumu kuu la OWMS na kwa kufanya hivi kutasaidia kuchukua hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa kwa haraka na hivyo kuepusha madhara ambayo yangeweza kutokea na kuisababishia hasara Serikali.

Akizungumzia utoaji wa taarifa, Dkt. Luhende aliwakumbusha Mawakili jumla ya mashauri mapya yaliyopokelewa na kuendeshwa kwa wiki hiyo pamoja na vikao walivyohudhuria ili OWMS iweze kufahamu kinachoendelea katika Ofisi za mikoani.

“Kila Ijumaa utatuandikia taarifa ya wiki hiyo, umepokea kesi mpya ngapi, umeendesha kesi ngapi; umehudhuria mashauri kwa usahihi hatua itakayosaidia OWMS kupata taarifa sahihi ili kuweza kupanga kazi za uendeshaji wa mashauri hayo kutokana na ukubwa wa kesi yenyewe na kwa kufanya hivyo tutaisaidia Serikali kushinda mashauri mengi kwa urahisi.

Dkt. Luhende aliwaasa Mawakili wasiotoa mrejesho baada ya kumaliza kazi



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na Mawakili wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki kikao kilichofanyika kwa njia ya mtandao kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Ofisi hiyo kilichofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam Desemba, 2022.*

wanaosimamia Ofisi za mikoani kuhakikisha wanatoa taarifa ya mashauri waliyoendesha kila Ijumaa itakayoonyesha vikao vingapi; umepokea barua ngapi”, alisisitiza Dkt. Luhende.

Aidha, aliwasihi Mawakili hao kutoa taarifa za uendeshaji wa walizotumwa kufanya hasa za uendeshaji wa mashauri ya Serikali katika Mahakama mbalimbali nchini na kuahidi kuwachukulia hatua stahiki

wale wote wataokasita kutoa taarifa hizo baada ya kurejea ofisini.

Kwa upande wake Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo aliwakumbusha Mawakili hao kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi pasipo na kujihusisha na masuala ya utovu wa nidhamu huku akisema kuwa hatasita kuchukua hatua stahiki za kinidhamu kwa Wakili yoyote atakayevunja sheria na taratibu za utumishi wa umma hasa katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali.



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali walioshiriki kikao kwa njia ya mtandao wakifuatilia masuala mbalimbali yaliyojadiliwa katika kikao hicho kama wanavyoonekana pichani kilichofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam Desemba, 2022.*



*Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza kwa makini Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi mbele) wakati akizungumza na Mawakili hao kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Ofisi hiyo kwenye ukumbi wa Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam Desemba, 2022.*

# Watendaji Tumieni Mawakili wa Serikali

Serikali imewataka watendaji wakuu Serikalini kuhakikisha wanawatumia ipasavyo Mawakili wa Serikali waliopo ndani ya mamlaka zao kabla ya kufanya maamuzi katika kuchakata mambo yote yanayohitaji miongozo ya kisheria na utawala bora.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi wakati wa uzinduzi wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika Septemba, 2022 jijini Dodoma na kusema wapo baadhi ya watendaji waliopewa dhamana kufanya maamuzi kwa niaba ya Serikali bila kuzingatia sheria.

"Mara nyingi Mawakili wa Serikali wamekuwa wakishirikishwa baada ya mashauri kufunguliwa dhidi ya Serikali katika vyombo vya maamuzi, na kama haitoshi, mara nyingi Mawakili wa Serikali wamekuwa wakikosa ushirikiano wa dhati kutoka kwa maafisa wa Serikali hususan pale maafisa hao wanapohitajika kwenda kutoa ushahidi na hivyo kusababisha Serikali kupoteza kesi nyingi katika vyombo vya maamuzi,"



**Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi**
Mwanasheria Mkuu wa Serikali



**Bi. Mary Makondo**
Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria

alisema Jaji Dkt. Feleshi.

Dkt. Feleshi alisema kuwa Mawakili wa Serikali wamekuwa wakipata wakati mgumu wakati wa kuitetea Serikali katika mashauri ambayo ni dhahiri yalipaswa kushughulikiwa kabla ya kupevuka na kufikishwa mahakamani au pale inapodhihirika kuwa haki ipo upande wa wadai.

Alisema kuwa miongoni mwa mambo yanayosababisha kesi za madai zinazoihusu Serikali na wadaawa binafsi yakiwemo mabenki na kesi za uwekezaji kuchukua muda mrefu kumalizika katika vyombo vya maamuzi na kufanya haki isipatikane kwa wakati ni Mawakili wa Serikali kutopata ushirikiano na ushahidi madhubuti kuthibitisha kesi zinazofunguliwa dhidi ya Serikali.

Awali, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo aliahidi kuwa Wizara itaendelea kufanya kazi kwa bidii na ueweledi ikishirikiana na Mawakili wa Serikali na wa taasisi nyingine ili kuhakikisha migogoro dhidi ya Serikali inapungua ndani na nje ya nchi.

Naye Wakili wa Serikali Rashid Said alisema kuwa baadhi ya Mawakili wa Serikali wamekuwa wakipata ugumu wa kutekeleza majukumu yao kwa sababu ya kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya watendaji wa taasisi zao ama wanaweza kushirikishwa tu endapo kumetokea ugumu katika masuala ya kisheria ambayo watendaji wanakuwa wameyatolea maamuzi.

Bw. Said alisema kuwa baadhi ya taasisi zimekuwa zikichelewa kutoa taarifa muhimu za uendeshaji wa mashauri yaliyopo mahakamani na kufanya Mawakili wa Serikali kupata wakati mgumu wa kuisimamia Serikali na kusababisha kuwa na mashauri mengi ambayo yangeweza kumalizika kabla ya kufika Mahakamani.

“Tuwaombe viongozi wetu kuhakikisha wanatutumia vizuri sisi Mawakili tuliopo ndani ya taasisi kwa kupata ushauri wanapoingia kwenye masuala ya kimkataba au wanapotaka kuvunja mikataba ili kujiepusha kuiingiza Serikali katika migogoro ambayo inaweza kuzuilika mapema,” alisema Said.



*Viongozi mbalimbali pamoja na Mawakili wa Serikali wakiwa kwenye ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete kwa ajili ya kushiriki Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali uliofanyika jijini Dodoma Septemba, 2022.*



# Baraza Kuweka Mahala pa Kazi Sehemu Salama

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende amewataka wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kutumia mafunzo wanayopatiwa kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa Baraza la wafanyakazi katika kuweka mahala pa kazi kuwa sehemu salama katika utendaji wa kazi na kuhakikisha kuwa wajumbe wa OWMS wanatekeleza majukumu waliyokasimiwa.

Dkt. Luhende aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku moja kwa wajumbe wa Baraza la Pili la Wafanyakazi wa OWMS yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu jijini Dodoma ambapo alisema kuwa mada tatu ziliwasilishwa kwa wajumbe hao ikiwemo wajibu na majukumu ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi; Kupitia Mkataba wa Baraza la Wafanyakazi; na umuhimu wa Baraza la wafanyakazi mahala pa kazi.

Aliwataka wajumbe kutumia fursa hiyo kuzijua hadidu za rejea ambazo zitawaongoza katika utendaji kazi wa kila siku na kutekeleza majukumu katika kipindi chote cha miaka mitatu watakachokuwa wajumbe wa Baraza hilo.



*Stanley Mahenge (kushoto) na Bi. Frazia Mulokozi (kulia), Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakifuatilia mada kuhusu umuhimu wa vyama vya wafanyakazi mahala pa kazi yaliyofanyika ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu jijini Dodoma Septemba, 2022.*

Alisisitiza kuwa Baraza la wafanyakazi ni chombo muhimu mahala pa kazi na kuwa sehemu salama ili kuleta tija katika utendaji kazi wa kila siku wa OWMS na aliwataka wajiandae kuhamia Dodoma mwaka huu.

"Mada inayohusu Mkataba wa Baraza la Wafanyakazi ni mahsusi kwa ajili ya kujenga uwezo na maarifa ya kujua kilichopo katika mkataba wetu kati ya Menejimenti na Baraza hili ikiwemo matarajio ya OWMS kutoka kwa wajumbe ukizingatia kuwa mkataba huu ni nyenzo muhimu katika utendaji kazi wetu kwa sababu unaainisha majukumu na mipaka yetu na matarajio kutoka kwa wafanyakazi," alisema Dkt. Luhende.

Akitoa mada ya umuhimu wa Baraza la Wafanyakazi, Katibu wa TUGHE Mkoa wa Dodoma, Samuel Nyungwa alisema kuwa ni muhimu kwa kila mtumishi kujiunga na chama cha wafanyakazi kwa sababu ni taasisi pekee ya wafanyakazi ambayo imeundwa kwa ajili ya kulinda na kutetea haki kwa kuweka sawa mahusiano ya kazi kati ya mfanyakazi na mwajiri wake mahala pa kazi.

"Vyama vya wafanyakazi ni wadau muhimu sana katika kulinda, kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi katika kuchangia jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba ustawi wa raia wake ambao ni wafanyakazi unaboreshwa na utendaji kazi unasimamiwa," alisema Nyungwa.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Sebastian Innosh aliwasilisha mada kuhusu umuhimu na uendeshaji wenye tija wa Baraza la wafanyakazi ambapo alisema kuwa mabaraza yanatakiwa kushauri na kujadili masuala muhimu ya taasisi; kutumia rasilimali watu na fedha kwa manufaa na uendelevu wa taasisi husika na taifa kwa ujumla; na kuimarisha mahusiano mema na kudumisha amani na utulivu mahala pa kazi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Katibu Mkuu wa TUGHE Taifa, Rugemarila Rutatina alisema kuwa mkataba wa Baraza la Wafanyakazi unaleta mafanikio na ushirikiano mahala pa kazi kwa kuwa unawaweka pamoja na kuwaleta karibu watumishi mahali pa kazi.

Akitoa maoni yake wakati wa mkutano huo, Athuman Zunda ambaye ni mmoja wa wajumbe wa Baraza hilo la OWMS alisema kuwa wamejifunza masuala mbalimbali kuhusu muundo wa Baraza hilo na idadi ya wajumbe wake kwa kuwa yeye ni mjumbe kwa mara ya kwanza kwenye Baraza hilo hivyo wamejifunza na kufurahishwa na namna ambavyo uongozi wa Baraza unavyofanya kazi ikiwa sambamba na suala la mjumbe wa kuchaguliwa kutoruhusiwa kutuma wawakilishi kwa kuwa wamechaguliwa na watumishi wengine ili kuwawakilisha na mjumbe wa kuchaguliwa asipohudhuria vikao vitatu (3) mfululizo bila ya kutoa taarifa kwa uongozi wa Baraza atakuwa amepoteza sifa ya kuwa mjumbe.



*Athumani Zunda, mjumbe mpya wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akichangia mada ya umuhimu wa Baraza la Wafanyakazi wakati wa mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Pili la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo yaliyofanyika Septemba, 2022 jijini Dodoma .*

# Tuwajibike kwa Pamoja kwa Maslahi ya Taifa






**Mhe. Jaji**
**Dkt. Eliezer Feleshi**
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Eliezer Feleshi (aliyeketi katikati) akiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu (kushoto), Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (kulia) katika picha ya pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Longopa (wa kwanza kushoto), Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Joseph Pande (wa pili kushoto), Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sarah Mwaipopo (wa pili kulia) na Mwandishi Mkuu wa Sheria (CPD) Onorius Njole (wa kwanza kulia) mara baada ya kufungua kikao cha pamoja kilichofanyika jijini Mwanza.*

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi amezitaka Menejimenti za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na uwajibikaji wa pamoja kwa kutumia uzoefu na ujuzi wa kila taasisi ili kuongeza thamani na kupata matokeo makubwa kwa maslahi ya Taifa.

Mhe. Jaji Dkt. Feleshi aliyasema hayo kwenye kikao cha pamoja cha Ofisi hizo kilichofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mwanza na kuwataka kusimamia uwajibikaji wa pamoja bila kuathiri nani

yupo wapi kwa kuwa wote ni familia moja na wanatekeleza majukumu kwa niaba ya Serikali.

"Sisi Wakurugenzi wa Idara mama za Ofisi hizi tatu tunatakiwa kuhakikisha kuwa idara na vitengo vingine saidizi zinafahamu majukumu yetu ili tuwe na uwajibikaji wa pamoja na kutumia uzoefu kwa kujengeana uwezo ili tuweze kupata matokeo makubwa na kuruka vihunzi na vikwazo mbalimbali kwenye taasisi zetu kwa maslahi mapana ya taifa", alisema Mhe. Dkt. Feleshi.

Alisema kuwa kikao hiki ni tukio la kihistoria kwa kuwa yapata miaka 3 kwa Ofisi hizi kuwa na kikao cha pamoja na sisi binadamu tunaishi kwa kujisahihisha ili tuwe na uelewa wa pamoja wa masuala yanayohusu muelekeo, maendeleo na maslahi ya Ofisi hizi na amevutiwa na namna masuala ya sheria yanavyobadilika kila siku na kuona umuhimu wa kutoa mafunzo ya kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwa Ofisi hizi ni kisima na chemchem ya mafunzo kwa Wakili wa Serikali.

"Sisi ni familia moja tumekutana kama familia tuongee masuala yanayotuhusu kwa mujibu wa majukumu ya msingi ya Ofisi hizi kwa hiyo tujenge uwezo wenye umahiri wa kutumikia taifa hili kwa niaba ya Serikali na wananchi kwa ujumla

Naye Mkurugenzi wa Mashtaka, ndugu Slyvester Mwakitalu alisema kuwa Ofisi hizi tatu ni muhimu sana kwa haki, amani na maendeleo ya taifa letu na Ofisi hizi zikilegea na kuwa na watumishi ambao hawatimizi wajibu wao taifa litapata madhara makubwa na kuwaumiza watanzania.

Ndugu Mwakitalu alisema kuwa Mawakili wa Serikali wasipokuwa na weledi na utaalamu wa kutosha watakuwa na mchango mdogo katika utekelezaji wa majukumu hivyo mafunzo ni muhimu ili kuwa na Mawakili wabobezi hasa kwenye maeneo ambayo tumekuwa tukifanya kazi zetu.

"Ninaamini kuwa tukiwa na vikao hivi mara kwa mara na tukajadili na kupeana majukumu ya kufikisha mwisho haya tunayojadili yatapunguza changamoto zilizopo na kufikiri namna ya kuzitatua ili kupata muafaka wa kila jambo". alisema Mwakitalu

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende aalisema kuwa Ofisi hizi zimekasimiwa majukumu makubwa ya kusimamia Sekta ya Sheria na utoaji haki hapa nchini hivyo ni muhimu kuelewa majukumu yetu na kutambua mafunzo yanayotakiwa katika kutekeleza majukumu yetu.

"Taifa hili lipo mabegani mwetu tumelibeba, tunalo jukumu zito linalohitaji kuwa na mifumo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu yetu. Miaka 60 hii ya Uhuru wetu ni vizuri kuelewa nafasi yetu katika majukumu haya tuliyopewa na tunahitaji ushirikiano ambao utatuwezesha kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi," alisema Dkt. Luhende.

Alisema kuwa ni vema kwa Ofisi hizi tatu kuwa na maono ya mbali zaidi kwa kufahamu mifumo, kutambua watumishi, aina ya mafunzo, ubobezi unaohitajika kwa Mawakili na utaratibu wa kutoa motisha kwa baadhi ya watumishi wanaotekeleza vizuri majukumu yao ili kuwapa ari ya kuendelea kufanya vizuri zaidi.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sarah Mwaipopo alimpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwakutanisha wajumbe wa Menejimenti wa taasisi hizo na kuwakumbusha kuendeleza umoja wao katika kutekeleza majukumu na chochote kinachotakiwa kufanyika kinapaswa kufanyika kwa pamoja.

Mwaipopo alisema kuwa ni muhimu kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kujenga taswira ya taasisi zetu na kujitafsiri

tukijenga na kusomeka vema kwa wadau wetu na tukabaini changamoto na namna ya kuzingatia maadili.

"Ni fursa kubwa sana ambayo tunatakiwa tuitendee haki kwa sisi wajumbe wa Menejimenti wa Ofisi hizi tatu kwa kuwa na kikao cha pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ana ndoto ya kuhakikisha Mawakili wa Serikali wanatekeleza majukumu yao ipasavyo na Ofisi hizi zinashirikiana kwa pamoja kusukuma mambo ya taasisi hizi tatu", alisema Mwaipopo.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Ofisi hizo na wajumbe hao wamedhamiria kuwa na muendelezo wa vikao vya namna hiyo ambavyo vitafanyika angalau mara tatu au nne kwa mwaka ili kutathmini mwenendo wa ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akiongea na Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo (hawapo pichani) kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kikao cha pamoja kuhusu majukumu ya Ofisi hizo kilichofanyika jijini Mwanza.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akiongea na Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo (hawapo pichani) kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kikao cha pamoja kuhusu majukumu ya Ofisi hizo kilichofanyika jijini Mwanza.*



*Mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu akitoa salamu kwa wajumbe wa Menejimenti (hawapo pichani) za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kikao cha pamoja kuhusu majukumu ya Ofisi hizo kilichofanyika jijini Mwanza.*



# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, TIArb Kushirikiana

*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyesimama katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi Sarah Mwaipopo (aliyesimama kushoto) na Rais wa Taaisisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi. Madeline Kimei (aliyesimama kulia) baada ya kumaliza kikao baina yao kilichofanyika kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania Bi. Madeline Kimei (hayupo pichani) alipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha.*

Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende ameahidi kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Usuluhishi Tanzania (Tanzania Institute of Arbitrators - TIArb) kwa lengo la kuhakikisha Sekta ya Usuluhishi nchini inaimarika zaidi.

Dkt. Luhende alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi. Madeline Kimei alipomtembelea Ofisini kwake jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha na kujadiliana namna ya kuendeleza ushirikiano baina ya Ofisi hizo katika tasnia ya usuluhishi nchini kwa kuwa wanategemeana katika utendaji kazi.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Dkt. Luhende alimpongeza Bi. Kimei kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuendeleza Taasisi hiyo kwa kushirikisha wadau ili waweze kupata haki stahiki kwa njia ya usuluhishi nchini na Ofisi yake iko wazi muda wote kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Usuluhishi ili iweze kusonga mbele.

Pia, aliongeza kuwa Serikali ni mdau mkubwa wa Sekta hii nchini na jambo linajidhihirisha kwenye bajeti ya Serikali ambapo kwa asilimia kubwa bajeti hiyo inakwenda katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kwenye maeneo mengine kama vile ujenzi ambako kunazalisha migogoro wakati



*Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi. Madeline Kimei akizungumza na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo na Mkurugenzi wa Usuluhishi wa Ofisi hiyo, George Mandepo (hawapo pichani) wakati wa ziara yake ya kujitambulisha kwa viongozi hao kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*

wa utekelezaji wake.

Amefafanua kuwa migogoro hiyo inapotokea inaleta haja ya uwepo wa usuluhishi badala ya kesi hizo kuingia kwenye mfumo wa Mahakama hivyo ni muhimu wakati wa usuluhishi kutengeneza mazingira ya kuona migogoro inamalizwa kwa wakati, haraka, na kwa kutumia gharama nafuu.

"Kumekuwa na gharama za uendeshaji wa migogoro hiyo kwa kuwa usuluhishi unachukua muda mrefu hivyo kuongeza gharama kwa wahusika na nia yetu ni kuhakikisha kuwa ushirikiano wetu unaenda kupunguza gharama hizi," alisema Dkt. Luhende.

Amesisitiza kuwa ni muhimu wasuluhishi wa migogoro wawe watu wenye taaluma husika, weledi, ujuzi, maadili, wazingatie kanuni za usuluhishi, walinde taswira ya taasisi husika, waepuke maslahi binafsi, wajenge imani ya taasisi kwa wadau na kulinda taswira yake katika uendeshaji wa migogoro mbali mbali kwa njia ya usuluhishi.

Kwa upande wake Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo amemshukuru Rais wa taasisi hiyo na amesisitiza kuwa ni muhimu kuwa vinara kwenye eneo la usuluhishi na Ofisi iko tayari kushirikiana na Taasisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuendeleza ushirikiano uliokuwepo tangu ulipoanzishwa na watangulizi wa Ofisi hizo ikiwemo kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya uendeshaji mashauri ya usuluhishi, mafunzo kwa Mawakili ikiwemo Kanuni mpya za usuluhishi za mwaka 2022 ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (kushoto) akimkabidhi Jarida la Wakili Mkuu Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi Madeline Kimei alipofika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujitambulisha.*

Naye Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi. Madeline Kimei alisema kuwa amefurahi kuona Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ina Idara ambayo imejikita kwenyemasualayausuluhishi ambayo inafanikisha utoaji huduma za usuluhishi nchini na Taasisi hiyo iko tayari kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kujenga ujuzi kwa Mawakili waliopo nchini ili wote kwa pamoja waweze kufikia kiwango cha kimataifa cha uendeshaji wa usuluhishi.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi wa Idara ya usuluhishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu George Mandepo alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa Ofisi hii eneo la usuluhishi lilihusika na masuala ya ujenzi ila kwa sasa mwelekeo umebadilika katika muktadha wa usajili, uendeshaji, taratibu, kanuni, ada, usajili, maadili na nidhamu ambapo inagusa maeneo mbali mbali ya usuluhishi hivyo ni muhimu kuwe na uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya usuluhishi ikiwemo kurithishana madaraka na kujenga uwezo kwa wasuluhishi chipukizi ili kulinda na kujenga taswira ya nzuri ya wasuluhishi, taasisi na wadau wanaohusika.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (kushoto) akimkaribisha Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi. Madeline Kimei alipowasili kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salam kwa ajili ya kujitambulisha.*



*Mkurugenzi wa Usuluhishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu George Mandepo akifafanua jambo kuhusu tasnia ya usuluhishi nchini wakati wa ziara ya Rais wa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania, Bi Madeline Kimei (hayupo pichani) ya kujitambulisha kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (hayupo pichani) walipokutana kwenye Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*

# Serikali Kuendeleza Sekta ya Sheria Nchini



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Sheria (hawapo pichani) kutoka Wizara mbali mbali, Taasisi za Umma, Mashirika ya Umma na Halmashauri zote nchini wakati wa kikao kazi kilichofanyika Jijini Dodoma.*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupanga mikakati ya kuendeleza Sekta ya Sheria nchini kwa ajili ya kuwatumikia watanzania.

Hayo yalielezwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende wakati akitoa salamu kwenye kikao kazi cha Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Sheria wa kutoka Wizara mbalimbali, Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Halmashauri zote nchini.

Dkt. Luhende aliongeza kuwa kikao kazi hicho kimewakusanya viongozi hao ili kupanga mikakati ya kuendeleza Sekta hiyo ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu ili kupata wanasheria wabobezi ndani ya Serikali ili

kuisaidia Serikali kutekeleza majukumu yake ambapo maelezo hayo yamejikita kwenye Kauli Mbiu ya Mwaka isemayo, "Utekelezaji wa Majukumu Unaozingatia Sheria ni Nyenzo Muhimu kwa Maendeleo ya Taifa."

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi ambaye ndiye muandaaji wa kikao kazi hicho alisema kuwa ya kuchukua hatua.

"Utumishi wa umma tunaoutaka kwenye Sekta ya Sheria ni kuhakikisha kuwa kila mtumishi wa umma wa kada ya sheria atumike kutokana na uwezo wake mahali alipo ambapo anaweza kuwa mwajiriwa wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali lakini akatumika kufanya kazi kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa Jaji Dkt. Feleshi.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi waliotoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ambao wameshiriki kikao kazi hicho, Shaban Ramadhan Abdallah, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuwa wamekuja kujifunza ili nao waweze kuiga na kwenda kutekeleza mashirikiano hayo baina ya Ofisi hiyo ya



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende (wa pili kushoto) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali wa Mikoa mbalimbali kutoka Ofisi hiyo wakati wa kikao kazi cha Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Sheria wa Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma, Mashirika ya Umma na Halmashauri zote nchini kilichofanyika jijini Dodoma. Wa tatu kushoto ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji. Dkt. Eliezer Feleshi.*

ni muhimu kwa viongozi hao kuelewa dira na dhima ya Ofisi wanazotumikia; kufanya tathmini nakujipima namna wanavyo tekeleza majukumu; kufanya uchambuzi wa wadau wa ndani na nje ya taasisi wanayofanyia kazi; kuweka mikakati endelevu ya kujengeana uwezo; kuepuka kujenga uadui na makundi; kufurahia kukoselewa na kufanyia kazi maeneo waliyokosolewa; na kuwa wadilifu ili wawe na nguvu siku hizi tunasoma kuwa mahiri na sio kusoma bora tu kusoma na mpaka sasa tuna jumla ya Mawakili wa Serikali 2,661 ambapo kati ya hao Mawakili 18 wana shahada ya uzamivu, 789 wana shahada ya uzamili, 863 wana astashahada ya juu na 855 wana shahada ya kwanza ya masuala ya sheria kwa mujibu wa takwimu zilizopo kwenye Mfumo wa Taarifa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (OAG-MIS) ambapo Mawakili hao wamejisajili," alisema Mhe. SMZ na za Tanzania Bara.

Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini, Slyvester Mwakitalu alisema kuwa baada ya kikao kazi hicho na Mkutano wa Mawakili wa Serikali utakaofanyika tarehe 29 na 30 Septemba, 2022 utawawezesha viongozi na washiriki kupata maarifa mapya pamoja na uzoefu kwa kuwa taasisi moja inafanya mambo yanayotekelezwa na taasisi nyingine kwa kuwa taasisi za Serikali zinafanya kazi kwa kutegemeana.



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali  Mhe. Jaji. Dkt. Eliezer Feleshi akifungua kikao kazi cha Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Sheria (hawapo pichani) wa Wizara mbalimbali, Taasisi za Umma, Mashirika ya Umma na Halmashauri zote nchini kilichofanyika Jijini Dodoma.*




*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Slyvester Mwakitalu, akizungumza na Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Sheria (hawapo pichani) kutoka Wizara, Taasisi za Umma, Mashirika ya Umma na Halmashauri zote nchini wakati wa kikao kazi chao kilichofanyika Jijini Dodoma.*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kigoma Yapata Gari

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) Mkoani Kigoma imefanikiwa kupata gari moja ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Akizungumza mara baada ya makabidhiano ya gari hilo yaliyofanyika katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Kigoma, Afisa Tawala Mwandamizi Geoffrey Annaniah alisema kuwa gari hilo limepatikana wakati muafaka kwani litasaidia utendaji wa kila siku na hivyo kupelekea kuongeza tija na kuleta matokeo chanya yatakayosaidia OWMS mkoani Kigoma kufikia malengo yake kwa wakati.

Aliongeza kuwa gari hilo ni moja ya jitihada za OWMS kuhakikisha kuwa inaboresha mazingira ya kufanyia kazi hasa ukizingatia ukubwa wa jiografia ya Mkoa huo ambapo Mawakili wamekuwa wakitumia muda mrefu kutoa huduma kutokana na umbali uliopo kutoka wilaya moja kwenda wilaya nyingine.



*Afisa Tawala Mwandamizi, Geoffrey Annaniah (kushoto) akimkabidhi nyaraka za gari Wakili Mfawidhi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Kigoma Allan Shija ikiwa ni ishara ya kumkabidhi gari hiyo kwa lengo la kuongeza ufanisi.*

Naye Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Kigoma Allan Shija ameishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia gari na kueleza kuwa gari hilo litasaidia kupunguza changamoto za kiutendaji zilizokuwepo awali kwa kuwa sasa litawasaidia kutembelea maeneo mbalimbali ndani ya mkoa huo ikiwemo yale maeneo yaliyokuwa hayafikiki kwa wakati.

"Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa mikoa mikubwa nchini, hivyo ujio wa gari hili utasaidia kutembelea wilaya za mkoa huu na kuhakikisha tunaisaidia Serikali na

wananchi kupata haki kwa wakati", alisema Shija.

Akielezea faida zitakazopatikana kutokana na ujio wa gari hilo, Shija alisema kuwa Mawakili wa Serikali mkoani Kigoma sasa watafika mahakamani kwa wakati tofauti na mwanzo ambapo iliwalazimu kutumia muda mrefu kwenda mahakamani kutokana na ukosefu wa usafiri wa uhakika hali iliyokuwa inapekelea watumishi hao kutumia muda mrefu kufika Mahakamani kwa kuchelewa.

Aidha, Shija alisema kuwa gari hilo litasaidia kuongeza tija hasa katika ubebaji na usambaji wa nyaraka mbalimbali kwa kuwa sasa nyaraka zote za Ofisi zitasambazwa kwa usalama na ufanisi zaidi na hivyo kuondoa uwezekano wa kuchelewa na kupotea kwa nyaraka zote zinazoihusu OWMS.

Shija alisema kuwa uwepo wa gari hilo utawasaidia sana Mawakili kuhudhuria mashauri mahakamani kwa wakati hasa pale wanapokuwa na shauri zaidi ya moja katika mahakama tofauti mkoani humo ikiwa ni pamoja na kushiriki mashauri mbalimbali na kutembelea maeneo yote yenye migogoro kwa wakati.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Kigoma inahudumia jumla ya Wilaya nane za Mkoa huo ambazo ni Wilaya ya Kigoma Manispaa, Kigoma DC, Kasulu Mjini, Kasulu DC, Kibondo, kakonko, Buhingwe na Uvinza.



*Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Kigoma Allan Shija (aliyesimama katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa ofisi hiyo mara baada ya kupokea gari kutoka kwa Afisa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu Mwandamizi Geoffrey Annaniah wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (wa kwanza kushoto) wa pili kushoto ni Mary Gunda, kutoka kulia ni madereva wa Ofisi Paul Mnene na Hassan Mrisho.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 321<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Chumba Na. 13 na 15<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |